



GRETCHEN WHITMER  
GOVERNOR

STATE OF MICHIGAN  
OFFICE OF THE GOVERNOR  
LANSING

GARLIN GILCHRIST II  
LT. GOVERNOR

## AMRI KUU YA UTENDAJI

No. 2020-21

### **Hitaji la muda la kuahirisha shughuli ambazo sio muhimu kwa kuendeleza na kulinda maisha ya watu**

Kirusi kipya cha Korona (COVID-19) ni ugonjwa unaohusiana na upumuaji na unaweza kusababisha kuugua vibaya au kifo. Ugonjwa huu unaletwa na aina ya kirusi cha Korona ambacho hapo awali hakikuhusiana na binadamu na kinachoambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Hatari ya kuugua vibaya au kufa kutokana na kirusi cha COVID-19 hutokea hasa miongoni mwa wazee na watu wenye maradhi sugu. Pia kuna kuongezeka kwa hatari ya maambukizi ya kirusi cha COVID-19 miongoni na watu ambao wanaokaa karibu na wengine. Hadi sasa hakuna chanjo iliyoidhinishwa au matibabu ya kuzuia ugonjwa huu.

Tarehe 10 mwezi wa tatu mwaka wa 2020, Idara ya Afya na Huduma za Watu ya Jimbo la Michigan iligundua visa viwili vya kirusi cha COVID-19 katika Jimbo la Michigan. Siku hiyo hiyo, nilitoa Amri Kuu ya Utendaji 2020-4. Amri hii ilitangaza hali ya dharura katika jimbo lote la Michigan chini ya sehemu ya 1 ya kifungu cha tano cha Katiba ya Michigan ya mwaka wa 1963, Sheria ya Usimamizi wa Dharura, 1976 PA 390, ilivyofanyiwa marekebisho, MCL 30.401-421, na Sheria ya Nguvu za Dharura za Gavana ya 1945, 1945 PA 302, ilivyofanyiwa marekebisho, MCL 10.31-33.

Sheria ya Usimamizi wa Dharurua inampa Gavana mamlaka mapana na majukumu “kukabiliana na hatari zinazotisha jimbo hili au watu wa jimbo hili kutokana na janga au jambo la dharura,” ambazo Gavana anaweza kutekeleza kupitia “amri kuu ya utendaji, matangazo maalum, na amri zilizoidhinishwa kisheria.” MCL 30.403(1)-(2). Vile vile, hii Sheria ya Mamlama ya Dharura ya Gavana ya 1945, imeeleza kwamba, baada ya kutangaza hali ya dharura, “Gavana anaweza kutoa maagizo, sheria na kanuni atakazoziona kuwa za lazima kulinda maisha na mali au kudhibiti hali ya dharura katika sehemu husika.” MCL 10.31(1).

Ili kupunguza kuenea kwa kirusi cha COVID-19, kuzuia kuzidiwa kwa mfumo wa utunzaji wa afya, kutoa nafasi ya kutengeneza vifaa hakiki vya upimaji, vyombo vya kupitisha hewa na vyombo vya kujikinga mwenyewe, ili kuzuia vifo visivyo vya lazima, ni jambo la busara na muhimu kuamrisha watu kukaa nyumbani au kwa makazi yao kadiri iwezekanavyo.

Amri hii itaanza kufanya kazi kuanzia tarehe 24 mwezi wa tatu, mwaka wa 2020, saa tsita na dakika moja mchana na itaendelea hadi tarehe 13 mwezi wa nne, 2020 saa tano na dakika hamsini na tisa za usiku.

Kwa kutumia maagizo ya Katiba ya Michigan ya mwaka 1963 na sheria ya Michigan, ninaamuru yafuatayo:

1. Amri hii lazima itafsiriwe kwa upana ili kuzuia watu kutoka nje kuenda kufanya kazi isiyohitajika katika kuendeleza au kulinda Maisha.
2. Ikitegemea mambo yasiyohusika katika sehemu ya 7, watu wote wanaoishi ndani ya jimbo la Michigan wanaamrisha kukaa nyumbani au makazi yao. Kwa kutegemea mambo hayo yasiyohusika, mikutano yote ya faragha na ya umma ya watu wa nambari yoyote wasio wa nyumba moja imepigwa marufuku.
3. Watu wote watakaotoka nyumbani mwao au makazi yao lazima wafuatilie maagizo ya kujitenga na umma yaliyopendekezwa na Vituo Vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, pamoja na kukaa futi sita mbali na watu wasio wa nyumba yako kwa upeo unaowezekana katika hali hiyo.
4. Hakuna mtu au shirika litaruhusiwa kuendelea na kazi inayowahitaji wafanyi kazi kutoka nyumbani kwao au makazi yao isipokuwa wafanyi kazi wanaohitajika kuendeleza au kulinda maisha au kufanya shughuli za kimsingi.
  - (a) Kwa ajili ya amri hii, wafanyikazi wanaohitajika kuendeleza au kulinda maisha wanafanuliwa kuwa “wafanyikazi wa miundombinu muhimu,” inavyolezwa katika sehemu ya 8 na 9.
  - (b) Kwa ajili ya amri hii, wafanyikazi wanaohitajika kufanya shughuli za kimsingi ni wale wanaolazimika kuwa kazini kuwezesha biashara au shughuli kudumisha orodha ya bidhaa na vifaa, kutunza wanyama, kudumisha usalama, kuchakata malipo ya wafanyikazi au kuwezesha wafanyi kazi kufanya kazi bila kulazimika kuenda mahali pao pa kazi.

Ni lazima biashara na viongozi wa kazi mbalimbali waamue ni baadhi gani ya wafanyikazi wao wanahitajika kufanya shughuli za kimsingi na wawajulishe wafanyikazi hao kuhusu uamuzi huo. Ni lazima biashara na viongozi wa kazi mbalimbali wawafahamishe wafanyikazi kuhusu uamuzi huo kwa maandishi, iwe ni kwa njia ya barua pepe, anwani ya mtandao wa umma au kwa njia nyingine inayofaa. Uamuzi huo, walakini, unaweza kuwasilishwa kwa mdomo hadi tarehe 31 mwezi wa tatu, 2020 saa tano na dakika hamsini na tisa za usiku.

5. Biashara na viongozi wa kazi mbalimbali wananoajiri wafanyikazi wa miundombinu ya kimsingi wanaweza kuendelea kufanya kazi kutoka mahali pao pa kazi ikitegemea masharti yafuatayo:

- (a) Kufuatana na sehemu ya 8 na 9, ni lazima biashara na viongozi wa kazi mbalimbali watambue ni baadhi gani ya wafanyikazi wao wanahitajika kufanya miundombinu ya kimsingi na kuwajulisha wafanyikazi hao kuhusu uamuzi huo. Ni lazima biashara na viongozi wa kazi mbali mbali wawafahamishe wafanyikazi kuhusu uamuzi huo kwa maandishi, iwe ni kwa njia ya barua pepe, anwani ya mtandao wa umma au kwa njia nyingine inayofaa. Uamuzi huo, walakini, unaweza kuwasilishwa kwa mdomo hadi tarehe 31 mwezi wa tatu, 2020 saa tano na dakika hamsini na tisa za usiku. Biashara na viongozi wa kazi mbalimbali hawafai kutambua:
- (1) Wafanyikazi wa huduma ya afya na afya ya umma
  - (2) Wafanyi kazi wanaofanya shughuli muhimu za serikali, ilivyoelezwa katika sehemu ya 6
  - (3) Wafanyikazi na watu waliojitolea kufanya kazi, ilivyoelezwa katika sehemu 9
- (d)
- (b) Shughuli ambazo sio za lazima katika kuendeleza na kutunza maisha, ambazo kwa kawaida hufanyiwa kazini ni lazima zihairishwe mpaka wakati mambo yatakapokuwa kawaida tena.
- (c) Biashara na viongozi wa kazi mbalimbali watakaendelea kuwa na wafanyikazi kazini ni lazima watekeleze maagizo ya kujitenga na umma na kufuata hatua nyingine za kusaidia kutunza wafanyikazi na wasimamizi. Maagizo na hatua hizi ni pamoja na, na labda zaidi ya:
- (1) Kuzuia nambari ya wafanyikazi katika sehemu ya kazi na kuhakikisha kuwa wafanyikazi watakaokubaliwa kazini ni wale tu wanaohitajika kuendeleza kazi ya miundombinu muhimu katika biashara au shughuli mbalimbali.
  - (2) Kuhimiza watu kufanyia kazi mbali na kazini kadiri iwezekanavyo.
  - (3) Kuhakikisha kuwa wafanyikazi na wasimamizi walioko kazini wanakaa umbali wa futi sita kutoka mtu mmoja hadi mwingine kadiri iwezekanavyo. Hili agizo linahusu wateja wanaosimama kwenye foleni.
  - (4) Kuongeza hali ya usafi na kutoambukiza katika vituo vya kazi ili kupunguza uwezekano wa wafanyikazi na wasimamizi kupata ugonjwa wa COVID-19, sawasawa na kufuata itifaki za kusafisha na kutoambukiza ikiwa kutapatikana na kisa cha COVID-19 mahali pa kazi.
  - (5) Kupitisha sera za kuzuia wafanyikazi kuingia mahali pa kazi ikiwa watakuwa na dalili za shida ya kupumua au wamekaribiana na mtu anayejulikana or kutuhumiwa kuwa na kirusi cha COVID-19.

- (6) Maagizo mengineyo yanayohusiana na kujitenga kwa umma na hatua za kupunguza uambukizi zilizopendekezwa na Vituo vya Kudhibiti Magonjwa.
6. Shughuli zote za serikali katika kiwango chochote (jimbo, kaunti au sehemu za karibu) zinazohitaji watu kuenda kazini au kusaidia biashara na shughuli mbalimbali ambazo sio za lazima katika kuendeleza au kutunza maisha zitahairishwa.
- (a) Kwa ajili ya amri hii, shughuli za lazima za serikali ni pamoja na shughuli zinazotendwa na wafanyikazi wa miundombinu muhimu, pamoja na wafanyikazi wa utelelezaji wa sharia, usalama wa umma, na wajibu wa kwanza.
- (b) Shughuli kama hizo pia ni pamoja na, lakini zinaweza kuzidi, usafirishaji wa umma, uokotaji na utupaji wa takataka, shughuli ambazo ni za lazima katika kuongoza na kusimamia uchaguzi, shughuli za lazima katika kusaidia wafanyikazi wa biashara na shughuli mbalimbali kuendeleza miundombinu muhimu, na udumishaji wa usalama na usafi kwenye viwanja vya kuchezea na kujistarehesha ili kuruhusu watu kupata burudani ya nje.
- (c) Kwa ajili ya amri hii, shughuli muhimu za serikali ni pamoja na shughuli za kimsingi, ilivyoelezewa katika sehemu 4(b). Wafanyikazi wanaofanya shughuli kama hizi hawaitaji kuteuliwa.
- (d) Kazi zozote za serikali zinazohitaji kufanyiwa mahali pa kazi lazima zitekelezwe kulingana na maagizo ya kujitenga na umma na hatua nyingine za kupunguza uambukizi ili kukinga wafanyikazi na walinzi ilivyoelezewa katika sehemu ya 5(c).
7. Maagizo ya pekee
- (a) Watu wanaweza kutoka nyumbani au kwa makazi yao na wakasafiri kama wanahitajika:
- (1) Kujihusisha na shughuli za inje, pamoja na kutembea, kutembea umbali mrefu, kukimbia, kuendesha baiskeli au shughuli za burudani zikifuatilia maagizo ya kujitenga kwa umbali wa angalau futi sita kutoka kwa watu wasioishi kwa nyumba moja na mtu yehusika.
- (2) Kufanya kazi zao kama wafanyikazi wa miundombinu muhimu baada ya kuteuliwa na waajiri wao. (Wafanyikazi wa miundombinu muhimu ambao hawahitaji kuteuliwa chini ya sehemu ya 5(a) wanaweza kutoka nyumbani kwenda kazini bila kuteuliwa.
- (3) Kutekeleza shughuli za kimsingi, ilivyoelezewa katika sehemu ya 4(b), baada ya kuteuliwa kufanya kazi kama hizo na waajiri wao.
- (4) Kufanya kazi muhimu za serikali ilivyoelezewa katika sehemu ya 6.

- (5) Kufanya kazi zilizo za lazima kwa afya na usalama wao, au afya na usalama wa familia au wanakaya (wakiwemo wanyama wanaokaa nyumbani). Kwa mfano, watu wanaweza kutoka nyumbani au makazi yao kwenda kununua madawa au kutafuta matibabu au huduma ya meno inayohitajika kushughulikia dharura ya kiafya au kuhifadhi afya na usalama wa mmoja wa kaya au familia (kukiwemo taratibu ambazo hazijahairishwa, kulingana na maagizo yaliyotolewa kuhusu taratibu ambazo sio za muhimu).
  - (6) Kupata huduma za lazima au vifaa wanavyohitaji wenyewe, wanafamilia au wanakaya na magari yao. *Ni lazima watu wajaribi kupata huduma hizi au vifaa hivi kupitia kwa kutumia huduma ya kupelekewa au kuwasilishiwa bidhaa kadiri iwezekanavyo.* Itakavyohitaji, walakini, watu wanaweza kutoka nyumbani au kwa makazi yao kununua bidhaa za vyakula na matumizi ya nyumbani, chakula cha kuchukua, petrol, vifaa vinavyohitajika kwa matibabu, na shughuli zingine za kimsingi zinazoinajika kwa makazi yao.
  - (7) Kuhudumia familia au mnyama wa kukaa ndani wa mmoja wa jamii.
  - (8) Kuhudumia Watoto, wategemezi, wazee, watu wenye ulemavu au watu walio kwenye hatari fulani.
  - (9) Kutembelea mtu aliye chini ya ulizi wa kituo cha huduma ya afya, kwenye makazi yake, au kituo kinachohudumia watu wengi, kadiri inavyokubaliwa.
  - (10) Kuhudhuria kesi za kisheria kwa sababu muhimu au za dharura ilivyoamrisha na mahaka.
  - (11) Kufanya kazi au kujitolea kusaidia kwa biashara au shughuli (zikiwemo shughuli za mashirika ya kidini na yasiyo ya kidini) ambazo zinatoa chakula, makazi, na mahitaji mengine ya kimaisha kwa watu walio na shida ya kiuchumi au watu wasiojiweza, watu wanaohitaji msaada kutokana na hali hii ya dharura, na watu walio na ulemavu.
- (b) Watu pia wanaweza kusafiri:
- (1) Kurudi nyumbani au kwa makazi yao wakitoka nje ya jimbo.
  - (2) Kutoka kwa jimbo hili kwenda nyumbani au kwingineko kwenye makazi.
  - (3) Kusafiri kati ya makazi mawili ndani ya jimbo hili.
  - (4) Inavyohitajika na watekelezaji wa sheria au amri ya mahakama, kukiwemo usafirishaji wa watoto kufuatana na mapatano ya ulinzi wa watoto.

8. Kwa ajili ya amri hii, wafanyikazi wa miundombinu muhimu ni wale ambao wameelezewa na Mkurugenzi wa Ulinzi wa Mtandao na Wakala wa Ulinzi wa Miundombinu wa U.S. katika mwongozo wake wa tarehe 19 za mwezi wa tatu, 2020 wa majibu kuhusu kirusi cha COVID-19 (yanayopatinana [hapa](#)). Wafanyikazi hawani pamoja na wafanyikazi katika kila sekta ifuatayo:
- (a) Huduma za afya na afya ya umma
  - (b) Watekelezaji wa sharia, usalama wa umma, na wajibu wa kwanza.
  - (c) Chakula na Kilimo
  - (d) Nishati
  - (e) Maji na maji machafu
  - (f) Usafirishaji na utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu.
  - (g) Kazi za umma.
  - (h) Tekinologia ya mawasiliano na habari, ikiwemo habari kutoka yombo vya habari.
  - (i) Shughuli nyinginezo za serikali zinazohusiana na maisha ya kijamii.
  - (j) Utengenezaji wa bidhaa muhimu.
  - (k) Vitu vyenye hatari
  - (l) Huduma za kifedha
  - (m) Usalama na usambazaji wa kemikali.
  - (n) Vituo vya kutengeneza vifaa vya ulinzi.
9. Kwa ajili ya amri hii, wafanyikazi wa miundombingu muhimu ni pamoja na:
- (a) Wafanyikazi wa huduma za utunzaji watoto (wakiwemo wafanyikazi wanaohudumia watoto katika vituo vya kutoa misaada wakati wa janga), kwa kiwango kinachohitajika tu ili kuhudumia watoto au wategemezi wa wafanyikazi wa miundombinu muhimu ilivyofafanuliwa katika amri hii. Kundi hili linahusisha watu (walio na leseni na wasiokuwa nayo) ambao wamepanga kutunza watoto au wategemezi wa wafanyikazi wa miundombinu muhimu.
  - (b) Wafanyikazi katika vituo vilivyoteuliwa kuuza na kusambaza ilivyoelezewa hapa chini.
    - (1) Biashara au shughuli ambayo imeajiri wafanyikazi wa miundombinu muhimu wanaweza kuteua wauzaji, vituo vya usambazaji au watoa huduma ambao kazi yao inahitajika ili kuwezesha, kusaidia au

kurahisisha kazi ya wafanyikazi wa miundombinu muhimu.

- (2) Hawa wauzaji, vituo vya usambazaji au watoa huduma wanaweza kuteua wafanyikazi kuwa ni wafanyikazi wa miundombinu muhimu *ikiwa tu* wafanyikazi hao wanahitajila ili kuwezesha, kusaidia au kurahisisha kazi ya wafanyikazi wa miundombinu muhimu katika biashara au shughuli za asili.
  - (3) Wauzaji, vituo vya kusambaza, na watoa huduma walioteuliwa wanaweza vile vile kuteua wauzaji, vituo vya usambazaji na watoa huduma zaidi ikiwa shughuli zao zinahitajika ili kuwezesha, kusaidia au kurahisisha kazi ya wafanyikazi wao wa miundombinu muhimu.
  - (4) Hao wauzaji, vituo vya usambazaji, na watoa huduma zaidi walioteuliwa wanaweza vile vile kuteua wauzaji, vituo vya usambazaji na watoa huduma kuwa wafanyikazi wa miundombinu muhimu *ikiwa tu* hao wafanyikazi wanahitajika ili kuwezesha, kusaidia au kurahisisha kazi ya wafanyikazi wa miundombinu ya wauzaji, vituo vya usambazaji, au watoa huduma waliowateua.
  - (5) Biashara, shughuli, wauzaji, vituo vya usambazaji na watoa huduma ni lazima wawafahamishe waliowateua kwa maandishi iwe ni kupitia kwa baura pepe, mtandao wa umma, or kwa njia nyingine. Uteuzi huo unaweza kufanywa kwa mdomo hadi tarehe 31 mwezi wa tatu, 2020 saa tano na dakika hamsini na tisa usiku.
  - (6) Biashara, shughuli, wauzaji, vituo vya usambazaji, na watoa huduma watakao tumia mamlaka yao ya kuteua vibaya wataadhibiwa kulingana na sheria.
- (c) Wafanyikazi katika tasnia ya bima, ikiwa tu kazi yao haiwezi kufanyika kwa simu au mbali na kazini.
- (d) Wafanyikazi na watu wanaojitolea kusaidia kwa biashara naushughuli(zikiwemo shughuli za mashirika ya kidini na yasiyo ya kidini) ambazo zinazotoa chakula, makazi, na mahitaji mengine ya kimaisha kwa watu walio na shida ya kiuchumi au watu wasiojiweza, watu wanaohitaji msaada kutokana na hali hii ya dharura, na watu walio na ulemavu.
- (e) Wafanyikazi wanaofanya majukumu muhimu katika vyama vya wafanyikazi, wakiwemo wale ambao wanasimamia fedha za afya na ustawi na wale ambao wanafuatilia ustawi na usalama wa wanachama ambao ni wafanyikazi wa miundombinu, iwapo usimamizi na ufuatiliaji huo unaweza kufanyika kwa simu au mbali na kazini, inapowezekana.
10. Hakuna kitu chochote katika amri hii kitachukuliwa kuwa cha muhimu zaidi kushinda amri kuu ya utendaji au maelekezo yanayotumika kwa wakati huu, ila tu amri hii imeweka vikwazo vikali kwa kazi inayotendewa kazini, kwa shughuli na mahusiano. Kulingana na maelelezo yaliyotelewa hapo awali, mahali pa ibada, patakapotumika kwa ibada, haitasababisha kuadhibiwa chini ya sehemu ya 14

11. Hakuna kitu chochote katika amri hii kinafaa kuchukuliwa ya kuwa kinaingilia au kukiuka mamlaka ya idara ya sheria au idara ya mahakama kwa kutekeleza majukumu yao ya kisheria au kutumia mamlaka yao.
12. Amri hii itatekelezwa kuanzia tarehe 24 Machi, 2020 saa sita za asubuhi na itaendelea hadi tarehe 13 Aprili saa tano na dakika hamsini na tisa za jioni.
13. Gavana atathatmini kama hii amri itahitajika kuendelea kutumika kabla ya wakati ulioweka kumalizika. Ili kuamua kama anahitaji kudumisha, kuongeza au kulegeza vikwazo, atatumia, kati ya vitu vingine, (1) habari kuhusu maambukizo ya kirusi cha COVID-19 na kiwango ambacho ugonjwa huu unaambukizwa; (2) kama kuna watu wa kutoa matibabu wa kutosha, vitanda vya hospitali na vifaa vya kusaidia katika kupumua vitakavyotimiza mahitaji ya matibabu yanayotarajiwa; (3) upatikanaji wa vifaa vya kinga kwa wafanyikazi wa huduma ya afya; (4) uwezo wa jimbo kupima visa vya kirusi cha COVID-19 na kutenga watu walioambukizwa; na (5) hali ya kiuchumi katika jimbo.
14. Kulingana na MCL 10.33 na MCL 30.405(3), mtu akikaidi sheria hii kwa hiari, atashitakiwa.

Imetolewa chini ya mkono wangu na Nembo Kuu ya Jimbo la Michigan.

Tarehe: Machi 23, 2020

Saa: 10:39 asubuhi



GRETCHEN WHITMER  
GAVANA

Gavana:

---

WAZIRI WA SERIKALI YA JIMBO